SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

# ZANZIBAR



# Mashirika, Taasisi za Umma Zanzibar zajivunia mafanikio




WASILIANA NASI

info@trosmz.go.tz
https://trosmz.go.tz/

Msajili Wa Hazina Zanzibar


ZIC Zanzibar Insurance Corporation | ZMUX | PBZ BANK | ZECO | ZHSF | ZASCO | ZAWA Zanzibar Water Authority | ZBC | ZAA Zanzibar Airports Authority | ZICTIA | ZHC Zanzibar Housing Corporation

# Mashirika, Taasisi za Umma Zanzibar zajivunia mafanikio

- Msajili wa Hazina Sanya abainisha mafanikio ikiwemo kupanda kwa gawio la serikali, asisitiza dhamira na malengo ya Rais Dk. Mwinyi lazima yatimizwe



"Uwepo wa Mashirika ya Umma ni kichocheo cha maendeleo ya Uchumi". Hii ni kauli mbiu inayotumiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kuonyesha umuhimu wa mashirika na taasisi za umma katika maendeleo ya nchi.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amekuwa mstari wa mbele kuchagiza mafanikio makubwa ya mashirika na taasisi za umma kutokana na maono yake.

Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inayoongozwa na Waheed Ibrahim Muhammed Sanya imemtaja Dk. Mwinyi kuwa kielelezo cha mafanikio na utendaji wa mashirika na taasisi za umma ikiwemo kuongezeka kwa gawio la serikali kwa mashirika hayo kutoka sh. bilioni 5.8 hadi sh. bilioni 13.7.

Pia, miaka minne ya Rais Dk. Mwinyi imekuwa kwa mashirika hayo ikiwemo kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar ambayo imekuwa na dira na miongozo ya kusimamia mashirika na taasisi kwa kutoa miongozo, kuanzishwa kwa mifumo ya teknolojia ya ununuzi na utunzaji wa mali.

Akizungumza na jarida la Hazina Zanzibar kuhusiana na miaka minne ya Rais Dk. Mwinyi mjini Unguja, Msajili wa Hazina wa Zanzibar, Sanya alisema Rais Dk. Mwinyi amekuwa mstari wa mbele kuleta mageuzi ya kiutendaji kwa mashirika ya umma ikiwemo kuanzisha ofisi hiyo, wanatimiza malengo na dira ya maendeleo.

Alisema uwepo wa ofisi hiyo ambayo awali ilikuwa haipo imekuwa chachu kubwa na kupitishwa kwa sheria ya kuanzishwa kwake mwaka 2021 na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Rais Dk. Mwinyi Oktoba 2021 imekuwa na mafanikio makubwa kwa mashirika.

"Kabla ya hapo kazi zinazohusu shughuli zinazoongozwa na kusimamiwa na Ofisi hii zilikuwa zinasimamiwa na taasisi za umma kwa mifumo ya taratibu zilizowekwa (sio kwa sheria). Dk. Mwinyi na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum wamekuwa na mchango mkubwa wa mafanikio yaliopo sasa," alisema.

**MAHOJIANO BAINA YA MSAJILI SANYA NI KAMA IFUATAVYO**

**SWALI:** Ofisi ya Msajili Hazina Zanzibar imekuwa mstari wa mbele katika usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma. Unaweza kueleza mafanikio ya mashirika hayo na faida waliyotengeneza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi cha miaka minne ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi?

**Jibu:**

Kwanza tunakushukuru kuja kututembelea na kupata uelewa wa masuala mbalimbali kuhusiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar. Pia, ni muhimu umma kuelewa kuwa Ofisi hii haikuwepo awali hadi hivi karibuni kuanzishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Ofisi hii toka ilipoanza hadi sasa ina miaka miwili baada ya kupitishwa kwa sheria ya kuanzishwa kwake mwaka 2021 na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Oktoba 2021.

> Ofisi hii toka ilipoanza hadi sasa ina miaka miwili baada ya kupitishwa kwa sheria ya kuanzishwa kwake mwaka 2021 na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Oktoba 2021.

Kabla ya hapo, kazi zinahozuhusu shughuli zinazoongozwa na kusimamiwa na Ofisi hii zilikuwa zinasimamiwa na taasisi za umma zenyewe kwa mifumo ya taratibu ziliwekwa (sio kwa sheria) na uzoefu wa miaka iliopita.

Kwa maana hiyo, kazi ya awali ya Ofisi hii baada ya kuzaliwa kwake ilikuwa ni matayarisho ya ofisi, mahitaji, kupangilia muundo, kujifunza kwa walioanza kazi kama hii mapema katika nchi jirani na kwengine.

Hapa nataka nielezee shukrani za dhati kwa ndugu zetu wa Bara (Ofisi ya Msajili wa Hazina ya Jamhuri ya Muuungano) kwa sio tu kutusaidia, bali kwa mashirikiano na msaada mkubwa wa undugu waliotupa na kuweza kutambaa na sasa tumesimama na kuanza safari vizuri.

Hapa ningependa kumshukuru kwa dhati Msajili wa Hazina wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Ndugu Nehemiah Mchechu kwa kushirikiana na sisi vizuri.

Lakini lingine lililotupa moyo zaidi na kutushajiisha ni namna ambavyo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anavyotusaidia kwa ushauri na kuibeba Ofisi hii na mashirikiano mazuri na miongozo tunayopata kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya na wasaidizi wake, na viongozi wengine wa Serikali wanavyotupa mashirikiano na ushauri wenye tija.

Kinachonipa faraja zaidi mimi (Msajili wa Hazina Zanzibar) na wenzangu ni namna ambavyo Taasisi za umma zilivyotupokea na kwenda nao vizuri katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za Ofisi hii.

**Sasa turudi kwenye suala la msingi wa mafanikio,mafanikio ya mashirika ya umma ni kama yafuatayo:**

1. Mashirika ya Umma kupata Sheria namba 6 ya mwaka 2021 ambapo sheria hii imeweza Kuweka misingi mizuri ya Utekelezaji kwa Mashirika ya Umma pamoja na Taasisi za Umma kwa upande wa Usimamizi wa Mali za Umma.
2. Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kipindi hiki imeweza kutoa jumla ya Miongozo Mitano (5) ya Mashirika ya Umma na Miongozo Miwili (2) ya Usimamizi wa Mali za Umma ambayo miongozo hiyo imekua ni chachu ya kuimarisha utendaji kazi wa Mashirika hayo pamoja na Taasisi za Serikali.
3. Uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi. Kwa kipindi cha Miaka minne Uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi umekua ukipitia hatua mbali mbali hadi kupatikana kwa wajumbe kwa mfano Wajumbe wa Bodi kabla ya

# Taasisi za Umma Zanzibar zajivunia mafanikio



kuteuliwa kupitiwa kwa sifa zao na uzowefu wao kulingana na Boidi husika.

4. Kuongezeka kwa utoaji wa Gawio kwa Mashirika ya Uwekezaji kutoka TZS 5.8 Bilioni hadi kufikia TZS 13.7 Bilioni kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

5. Ushirikiano thabiti uliopo baina ya Mashirika ya Umma na Ofisi ya Msajili wa Hazina na kufanya taasisi hii kuweza kufikia malengo ya kuanzishwa kwakwe.

6. Kuanzishwa kwa Mifumo ya Usimamizi wa Mashirika ya Umma (OTRMIS) na Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Umma (ZGAMIS).

**SWALI;** Moja ya jukumu la Shirika la umma ni kutengeneza faida. Ipi mipango ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhakikisha mashirika hayo yanatengeneza faida kubwa kwa umma?

**Jibu:**

Serikali imeanzisha mashirika na taasisi za umma ili kupata ufanisi katika sekta mbalimbali na ziweze kuchangia mapato ya kuendesha shughui za Serikali na kupatikana fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na sio kuwa mzigo kwa taifa, yaani sio kufanya shughuli zake kwa hasara.

Katika kuhakikisha lengo hili linafikiwa kwa ufanisi tulianza na kutoa elimu juu ya kuwepo kwa Ofisi hii, malengo yake na kueleza kwa kutoa mifano ya namna wenzetu katika nchi mbalimbali walivyofaidika kwa kuwepo kwa Ofisi kama hii.

Binafsi na wenzangu tumefarijika na namna ambavyo taasisi za umma zinavyofanya kazi kwa ushirikiano na sisi. Tumefanya nao vikao mbalimbali, tumefanya tafiti za kupata takwimu zitazosaidia tujuwe tunakwenda vipi kwa salama na uhakika katika safari yetu.

Pia, tumetayarisha mfumo na miongozo juu ya matumizi ya fedha za umma, manunuzi, uuzaji wa mali za serikali na kuweka bayana nani anahusika na nini na namna gani manunuzi na mauzo ya mali ya serikali yatafanyika.

Katika hili tumetengeneza Muongozo ambao taasisi zote zimepatiwa na kwa hili tulikuwa na mafunzo maalum ya kuelimisha na kubadilishana ushauri.

Tayari pameanza kupatikana mafanikio na kwa sasa michango ya taasisi za umma kwa Hazina imekuwa mikubwa zaidi na mashirikka ambayo yalikuwa hayafanyi vizuri yameanza kurekebisha mfumo wa utendaji wake wa kazi na kuanza kuwa na hali nzuri.

Kimsingi jukumu kubwa la Mashirika ya Umma ni kufanya biashara na kutoa huduma, ambapo biashara ikifanyika uzuri na huduma ikipokelewa vizuri ndipo kunakopelekea kupatikana kwa faida.

Kwa hivyo, Msajili wa Hazina katika kuhakikisha mashikirika haya yanapata faida imejiwekea mipango thabiti ikiwemo:

1. Shirika kuweza kufanya biashara yenye tija,

2. Shirika kuweza kuhakikisha kua huduma inayotoa inawafikia wananchi ipasavyo,

3. Kuepuka matumizi mabaya ya Rasilimali fedha,

4. Kuajiri wafanyakazi wenye uwezo na wanaoendana na Malengo ya Mashirika ya Umma.

Ninaamini kwa dhati haitachukua muda mrefu kwa viwango vya taasisi zetu vya kuchangia vitapanda.

**SWALI:** Unaweza kueleza mikakati yako katika kuweka mifumo, sheria bora za uboreshaji utendaji wa menejimenti za mashirika ya umma na kujiendesha kibiashara.

**Jibu:**

Kama nilivyoeleza hapo juu mikakati yetu na mipango ni mingi. Ipo ya muda mfupi na ipo ya muda mrefu na tunachukua tahadhari ya kutofanya mambo mengi kwa wakati mmoja.

Ni vema kwenda mwendo wa kiasi badala ya kutaka kukimbia wakati uwezo wa kufanya hivyo haupo. Lakini kwa muhtasari tumeanza vema safari na tunaona mbele mwanga wa matumaini wa kupata mafanikio.

Hivi sasa unaona mabadiliko makubwa ya mashirika yetu, badala ya tu kutoa huduma muhimu kwa jamii, bali pia yameanza kujiendesha kibiashara na mzigo kwa Hazina kuanza kupungua.

Hata hivyo, Sheria ya Msajili wa Hazina nambari 6 ya mwaka 2021 Kifungu cha 6,7,8 na 9 vimenipa majukumu na uwezo wa kuyasimamia na kuyatekeleza kwa vitendo masuala ya Sheria , Sera,Miongozo na Maelekezo mbali mbali.

**SWALI;** Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia na kutathmini utendaji wa jumla wa Taasisi za Uwekezaji. Ipi mipango ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhakikisha uwekezaji unaofanyika unakuwa na maslahi kwa taifa?

**Jibu:**

Uwekezaji hivi sasa umeshika kasi katika kila sekta na tunafarajika kuliona hili kwa sababu uwekezaji una umuhimu mkubwa katika kukua kwa taasisi na nchi kujipatia maendeleo.

Tumetayarisha utaratibu katika miongozo tulioutoa kwa taasisi, baada ya kuwashirikisha wadau wote na kuchota uzoefu wa Ofisi kama yetu za nchi mbali mbali.

Hili tunalifanya kwa kutumia wataalamu wetu na wengine wa serikali na kushirikiana kwa karibu na Wizara inayosimamia Uwekezaji na Mamlaka ya Ukuzaji Uwekezaji Zanzibar (ZIPA). Tunafanya kazi pamoja kwa vile sote lengo letu ni moja, isipokuwa upo mgawanyo wa kazi za kufanya kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Katika kuimarisha utendaji kazi wa Mashirika, Ofisi ya Msajili wa Hazina inajua kua yapo baadhi ya Mashirika ya Umma yanaekeza Mitaji yao katika Biashara mbali mbali. Katika suala hili Ofisi inazingatia masuala mbali mbali kabla Mashirika ya Umma hayajenda kuekeza katika Biashara husika. Miongoni mwa vipengele vya kuzingatia ni pamoja na:

1. Upembuzi yakinifu wa Biashara inayotaka kufanyika,

2. Wazo la Biashara,

3. Aina ya Biashara itakayofanyika,

4. Gharama zitakazo tumika na Faida itakayopatikana na

5. Eneo ya Biashara hiyo itakayoenda kufanyika.

Ofisi ya Msajili wa Hazina ikijiridhisha na masuala hayo ndio hutoa kibali cha kuruhusu Shirika la Umma kuweza kufanya uwekezaji.

**SWALI;** Unaweza kueleza ushirikiano uliopo baina ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar katika

Serikali imeanzisha mashirika na taasisi za umma ili kupata ufanisi katika sekta mbalimbali na ziweze kuchangia mapato ya kuendesha shughuli za Serikali na kupatikana fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na sio kuwa mzigo kwa taifa, yaani sio kufanya shughuli zake kwa hasara.

# DKT. MWINYI KINARA



kuhakikisha mnatekeleza kwa vitendo dhana ya umoja na mshikamano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**JIBU**:

Ushirikiano wetu na Ofisi ya Msajili wa Hazina wa Jamhuri ya Muungano ni mkubwa na ninaweza kusema sio tu tunaridhika nao, bali tunaufurahia.

Tunafanya vikao vya pamoja vya kuelimishana, kubadilishana uzoefu na kushauriana. Wao wanaohudhuria mikutano yetu, ikiwa pamoja na ile ya mafunzo na sisi tunahudhuria yao.

Ushirikaino huu sio tu kwa viongozi wa hizi ofisi, bali hata kwa wafanyakazi wa kada za kati na chini wa vitengo mbali mbali.

Kwa sasa mashirikiana ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ya Tanzania Bara na Zanzibar upo mkubwa ,kwani

1. Kunahati ya mashirikiano baina ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara na Zanzibar (MOU),
2. TR Zanzibar amekua Wakishiriki katika Vikao mbali mbali vya Mashirika kwa Mfano Siku ya Gawio ambayo kwa mwaka huu ilifanyika jijini Arusha. Watendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kuweza kushiriki mafunzo ya ndani Tanzania Bara na Watendaji TR Bara wameweza kutoa Mafunzo ya kiutendaji kwa Watendaji wa TR Zanzibar Unguja.
3. Kushirikiana kwa uandaaji wa Miongozo mbali mbali na uandaaji wa Mfumo wa Mashirika unaoitwa OTRMIS.

**SWALI;** Moja ya changamoto zinazolikabili taifa kwa sasa ni ajira kwa vijana. Ni kwa kiwango gani mashirika ya umma yamesaidia katika kupunguza tatizo la ajira?

**Jibu:**

Suala hili kwa kweli nitakudanganya kama nitakupa jawabu ya uhakika. Hata hivyo, tunaendelea kufanya utafiti na tumeshauri katika miongozo tunayoitoa na katika mafunzo na semina tulizofanya juu ya umuhimu wa kila taasisi ya umma kuchangia kupunguza tatizo hilo na hasa kwa kutoa kipaumbele kwa vijana wa Zanzibar wakati zinapochomoza nafasi za ajira.

**YAFUATAYO YAMESAIDIA KUPUNGUZA TATIZO LA AJIRA:**

1. Kuruhusu uwekezaji katika Sekta binafsi,
2. Kuwawezesha vijana kwa upatikanaji wa mitaji kupitia Idara ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi,
3. Kuongeza fani mbali mbali za kujiajiri katika vyuo vya amali,
4. Kupunguza Kodi zisizozalazima kwa wajasiria mali,
5. Kutolewa kwa Mikopo kwa baadhi ya wajasiria Mali kulingana na shirika husika yakiwemo ZAFICO, ZASCO, PBZ,
6. Mashirika yameweza kuajiri watendaji wa Kudumu na kwa Muda.

**SWALI:** Mpango uliopo kwa sasa ni kuyawezesha mashirika ya umma kujiendesha kwa faida na kuwekeza nje ya mipaka ya Tanzania. Nini kauli yako katika hili?

**Jibu:**

Kama ilivyoeleza hapo awali tunayo mipango ya muda mfupi na muda mrefu. Hivi sasa tumejikita zaidi kujiimarisha hapa ndani kwa kuweka mifumo mizuri na miongozo ya utendaji kazi na huku tukifanya tathmini za kila robo mwaka.

Uwekezaji nje ya nchi ni kazi za taasisi na kazi yetu ni kutathmini tija itayoweza kupatikana na kushauriana.

Kwa sasa ndio tunaendelea kupata takwimu na kuzifanyia kazi na baadaye ndio tunaweza kutoa ushauri wenye uhakika. Hii ni kazi inayohitaji kufanyika kwa kitaalamu baada ya kufanyika utafiti wa kina na sio kurupuka tu.

Kwa hivyo, mimi kama Msajili wa Hazina naipongeza sana fursa hii kutoka na kwamba utaweza kutanua uwekezaji zaidI nje ya Mipaka ya Zanzibar na ndilo lengo la Serikali kwa Mashirika ya Umma.

Kwani kufaya hivyo kutapelekea sasa Shirika kuzidi kujitengemea zaid na ule mtaji ulioelekezwa na Serikali kurudi katika njia ya Gawio. Ambapo tayari baadhi ya Mashirika ya Uwekezaji Zanzibar tumeanza kuyashauri kununua Hisa katika Kampuni za Nje ya Zanzibar.

**SWALI:** Ipi mipango ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuyawezesha mashirika kushiriki katika uwekezaji eneo la uchumi wa buluu?

**Jibu:**

Uwekezaji wa eneo la Uchumi wa Buluu ni mtambuka, yaani karibu kila sekta inahusika. Kwa mfano Wizara ya elimu kutoa mafunzo juu ya njia bora za uvuvi, faida ya kulinda matumbawe na athari za kuharibu mazingira ya fukwe na bahari.

Tunacho shauri ni kila kinachofanaywa kiwe na sababu za msingi za kukifanya, kifanywe baada ya kufanywa utafiti na majaribio ambayo matokeo yake yatatoa sura ya nini kitegemewe na pawepo mashirikiano na sio kila taasisi kwenda njia yake kama safari ya kila taasisi ni tafauti na ya mwenzake.

Hapa ningependa kukumbusha kwamba na vyombo vya habari navyo vinapaswa kusaidia kutoa elimu ya uchumi wa buluu na kuelezea, kwa mfano, uzoefu wa uchumi wa buuu uliopatikana nchi mbali mbali, na hasa simulizi za mafanikio za uchumi wa buluu katika nchi mbali mbali.

**Sasa kwa mashirika ya umma:**

1. Kwanza kuhakikisha mashirika hayo yanafanya upembuzi yakinifu kwa namna gani Katika eneo la Uchumi wa Buluu eneo gani linaeza kuekeza,
2. Kuhakikisha kua uwekekzaji huo unaendana na Malengo ya Shirika,
3. Kuhakikisha kua Shirika lina Rasilimali watu wa kutosha na wenye ujuzi katika eneo la Uchumi wa Buluu,

**SWALI:** Karafuu ni moja ya zao la kihistoria na kimkakati kisiwani Zanzibar. Nini mipango na mikakati ya ofisi yako kuliwezesha Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kukuza soko la karafuu ili liendelee kuchangia pato la taifa?

**Jibu:**

Ofisi ya Msajili Hazina inaelewa kuwa zao la Karafuu ni zao la Utii wa Mgongo kwa Uchumi wa Zanzibar na jukumu hili ni kweli limepewa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC). Kwa kua kuna changamoto mbali mbali ambazo zinakabili zao hili pamoja na Shirika hili hivyo Ofisi ya Msajili wa Hazina inamikakati ifuatayo katika kuliwezesha Shikika hili na kusimamia zoa la Karafuu.

1. Kuimarisha uzalishaji wa zao hili
2. Shirika kulipatia fedha zaidi ilikuhakikisha kwamba kila msimu zao hili linanunuliwa
3. Kutanua na kuongeza wanunuziwa zao hili nje ya mipaka ya Zanzibar kupitia ZSTC
4. Kushrikiana na vyombo vyengine vya ulinzi na Usalama ikiwemo zaidi KMKM katika kuhakikisha kua inakomesha Magendo ya zao hili
5. Kutoa elimu kwa wakulima wa zao hili katika kuhakikisha kua wanauza karafuu zao katika shirika la ZSTC kwa maendeleo ya Taoifa na jamii kwa ujumla.

Miongoni mwa maeneo tuliyoyakusanyia takwimu ni shirika la ZSTC. Tumejaribu kuchambua changamoto zake, tumeshauriana na uongozi wake na tumetoa maendekezo yetu ya nini kifanyike ili ZSTC iwe sio imara tu, bali iweze kutoa mchango mkubwa zaidi kwa maendeleo ya nchi yetu.

**SWALI:** Zanzibar inavuma kwa kuwa na fursa mbalimbali za utalii wa kipekee. Ipi mipango ya ofisi yako katika kukuza utalii visiwani humo?

**Jibu:**

Zanzibar inayo nafasi kubwa ya kukuza sekta ya utalii kwa vile ina vivutio vingi na sifa za ukarimu wa watu wake. Lakini kuwa na kitu kizuri jambo moja na kukitumia vizuri na kuwa endelevu ni jengine.

Katika miongozo yetu kwa taasisi zinazohusika na utalii kwa njia moja au nyengine tumeligusia na tumekuwa tunatoa mafunzo ya kutafuta njia nzuri za kukuza sekta hiyo bila ya kuathiri mazingira yetu na utamaduni wetu, mila na desturi za maisha ya kila siku.

Kwa kuwa Utalii ni Sekta mtambuka, hivyo Ofisi ya Msajili wa Hazina inayo nafasi katika kuhakikisha inakuza utalii visiwani Zanzibar katika njia zifuatazo:

1. Kuwa na Utamaduni kama Ofisi kufanya utalii wa ndani,
2. Wageni wanaopokewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina mbali na majukumu wanayokuja nayo pia kuhakikisha wanapelekwa katika maeneo mbalimbali ya vivutio vya utalii ikiwemo maeneo ya kihistoria,
3. Hata Mashirika nayo yakiona upo uwekezaji mzuri na wenye faida katika sekta ya Utalii yanaruhusiwa kuwekeza kwa kuzingatia vigezo na masharti ya uwekezaji.

# PONGEZI

**Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea wa nafasi ya Urais Zanzibar mwaka 2025**

***"Uwepo wa Mashirika ya Umma ni kichocheo cha maendeleo ya Uchumi"***



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

**Dkt. Hussein Ali Mwinyi**


SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR







# YATEKELEZA KWA VITENDO












**“Ni vyema kila Shirika au Taasisi za uwekezaji za Umma zikajitathmini kujua changamoto wanazokabiliana nazo katika uendeshaji wa Taasisi zao na kupanga mipango ya namna ya kutatua changamoto hizo ili kuleta ufanisi mkubwa katika uendeshaji wa Mashirika ya Uwekezaji wa Umma, si vyema kubaki na changamoto ambazo zinasababisha hasara kwa shirika au Taasisi.”**

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi




**"Azma ya Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ni kuleta mabadiliko kwa mashirika na taasisi za umma Zanzibar. Kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kimaendeleo kwenye Mashirika ya Umma hususan katika kutoa huduma bora kwa wananchi, kuhakikisha yanakamilisha malengo na mikakati ya Serikali iliyojiwekea."**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Mhe Dkt. Saada Salum Mkuya

# SMZ YAKOSHWA NA MASHIRIKA






# TAASISI ZA UMMA ZANZIBAR




MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua mchango mkubwa unaotolewa na Mashirika ya Umma na itaendelea kuchukua juhudi mbalimbali kuhakikisha Mashirika hayo yanafanya kazi kwa ufanisi mkubwa hapa nchini.

Amesema kwa kutambua umuhimu wa Mashirika ya Umma Serikali imechukua hatua ya kuanzishwa kwa Afisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar chini ya Sheria Namba 6 ya mwaka 2021 na kupewa jukumu la kuwa msimamizi mkuu na mmiliki pekee wa uwekezaji wa Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais amesema kuwepo kwa Afisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kumechangia kuleta mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa Mashirika ya Umma, utoaji wa huduma kwa wananchi na kuchangia kuongezeka kwa kwa mapato ya Serikali ambapo kwa mwaka 2022- 2023 Mashirika ya Umma yameweza kuchangia gawio la Shilingi za Kitanzania Bilioni 13.7.

Hemed amesema Shirika la Bandari limeweza kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa meli za mizigo katika bandari ya Malindi kupitia muwekezaji Afrikan Global Logistic(AGL) na kuchochea kuongezeka kwa mapato kutoka shilingi za Kitanzania Bilioni 5.5 hadi kufikia Bilioni 6 kwa mwezi kwa mwaka 2024.

Hemed amefahamisha kuwa Shirika la Bima la Zanzibar limepata mafanikio makubwa kwa kuendelea kutoa huduma bora na za kisasa kwa wananchi kwa kupitia Mifumo ya Tehama na kuchangia kukua kwa mapato kutoka Bilioni 19 kwa mwaka 2021 na kufikia Bilioni 130.74 kwa mwaka 2024.

## MAPATO

**Hemed amefahamisha kuwa Shirika la Bima la Zanzibar limepata mafanikio makubwa kwa kuendelea kutoa huduma bora na za kisasa kwa wananchi kwa kupitia Mifumo ya Tehama na kuchangia kukua kwa mapato kutoka Bilioni 19 kwa mwaka 2021 na kufikia Bilioni 130.74 kwa mwaka 2024.**

Sambamba na hayo amewaagiza viongozi wa Mashirika ya Umma kuendelea kuboresha Mifumo ya utendaji katika utoaji wa huduma ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu na kuendelea kukuza ushirikiano wa karibu kati ya viongozi na Afisi ya msajili wa Hazina kwa kutatua changamoto mbali mbali zinapotokezea.

Naye, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Saada Mkuya amesema kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kimaendeleo kwenye Mashirika ya Umma hasa katika kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuhakikisha yanakamilisha malengo na mikakati ya Serikali iliyojiwekea.

Dkt. Mkuya amesema azma ya Rais Dkt. Mwinyi ni kuhakikisha kupitia Shirika la Nyumba na Mashirika mengine Zanzibar inakuwa na mji wenye majengo ya kisasa yenye kukidhi huduma zote stahiki ambayo yataufanya Mji wa Zanzibar kuwa wenye haiba na muonekano mzuri utakaoitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi.

Dkt. Saada amewataka wananchi kupuuza uvumi unaotolewa na wasioitakia mema Zanzibar na badala yake kuyatangaza mambo mazuri ya kimaendeleo yanayofanywa na Rais Dkt Hussein Mwinyi kwa Wazanzibari wote.

Kwa upande wake, Msajili wa Hazina Zanzibar, Waheed Mohammed Sanya amesema Afisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imefanikiwa kuyaunganisha Mashirika 18 ya umma yaliyopo Zanzibar ambayo yanafanya kazi kwa ushirikiano jambo ambalo linaifanya Afisi ya Msajili wa Hazina kupiga hatua kimaendeleo katika kipindi kifupi tangu kuanzishwa kwake.

Waheed amesema Wiki ya Mashirika ya Umma itakuwa endelevu na itafanyika kila mwaka lengo ikiwa ni kuyaweka pamoja Mashirika na kujadili mafanikio lakini pia kutafuta njia muafaka za kupata utatuzi wa changamoto mbali mbali zinazoyakabili mashirika hayo.

# Mchechu aahidi ushirikiano na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar

MSAJILI wa Hazina Tanzania Bara, Jeremiah Kyando Mchechu amesema ushirikiano kati ya Ofisi ya Msajili Bara na Zanzibar ni njia moja ya kuleta mabadiliko ya kukuza uchumi nchnii.

"Tunaenda kubadili sharia ili tuendane na kasi ya uchumi wanayoitaka viongozi wetu" alifafanua

Amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imo katika mkakati wa kukuza na kuimarisha Uchumi wa nchi kwani ukuaji wa Uchumi unaenda kwa kasi hivyo ni vyema kuwa makini katika kusimamia na kuweka mpango mkakati ili kufikia malengo.

Amesema wameamua kubadilishana uzoefu na kupeana ujunzi wa kiutendaji katika kazi zao za kila siku ikiwa utekelezaji wa makubaliano waliyotiliana saini Aprili 2023 kusaidia kuleta ufanisi.

"Ushirikiano kati yetu katika utendaji wa kazi zetu ni jambo lisiloepukika kwa vile sote tunafanya kazi moja ya kusimamia mali za umma"alifafanua Mchachu.

Msajili Mchachu ameongeza kuwa ni wajibu wao kuhakikisha Taasisi zote za Serikali zinafanya vizuri katika kusimaia mali za Umma na kuchukua hatua kwa mujibu wa sharia endapo taasisi hizo zitakwenda kinyume na sharia za usimamizi wa mali za umma.

Katika hatua nyingine, Mchechu ameeleza kuwa katika kuimarisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Wasajili wamekubaliana kuongeza weledi wa katika kusimamia mashirika kwa manufaa ya umma wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ameongeza kuwa pia wameamua kubadilishana wafanyakazi na uzoefu wa watendaji kitaalamu pamoja na kuwa kioo cha ufanisi wa utendaji kazi kwa kushiriki kikamilifu katika kudumisha Muungano wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Naye, Msajili wa Hazina Zanzibar Waheed Muhammad Sanya amefahamisha kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kwa sasa inasimamia mashirika 18 na imejipanga kuhakikisha mashirika hayo yanaleta tija kulingana na malengo ya kukuza uchumi kutokana na maono ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Mwinyi.







# MAFUNZO





# Msajili Sanya atoa maagizo kwa watendaji

MSAJILI wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waheed Ibrahim Muhammed Sanya amewataka watendaji wa Taasisi mbalimbali na mashirika ya umma kushirikiana na Ofisi hiyo ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi.

Akifungua mkutano wa kuwajengea uwelewa watendaji Wakuu wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma katika Ukumbi wa Zura Maisara amesema kikao hicho kitawawezesha kufahamu majukumu yao pamoja na kujua Ofisi ya Msajili wa Hazina ina nafasi gani katika utendaji wao.

Amesema Taasisi ya hazina ni Taasisi kubwa inayofanya kazi kwa karibu na taasisi nyingi za Serikali hasa zinazozalisha hivyo ni wajibu wao kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo nchini.

Amesema kuwa lengo la mkutano huo ni kujenga uelewa kwa watendaji wa taasisi hizo juu ya kazi zinazofanya na ofisi ya Msajili wa hazina pamoja na kuwapatia fursa ya kuwasilisha changamoto zinazowakabili katika taasisi zao na kuzipatia ufumbuzi.

Akiwasilisha mada ya mahusiano baina ya Ofisi na Mashirika ya umma na mpango kazi wa ofisi hiyo Kaimu Mkuu wa Mashirika ya Uwekezaji ya Umma, CPA Mussa Ali Juma amesema kuwa Serikali inatoa gawio kwa taasisi zake kupitia uchangiaji wa Taasisi hizo ili kuendeleza utendaji kazi wao na kuleta maslahi kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Akitoa ufafanuzi kuhusu ofisi ya Msajili wa hazina Mussa amesema kuwa kuna haja ya kufanya muongozo mmoja katika Taasisi kutokana na uwepo wa miundo tofauti katika taasisi hizo.

Amesema lengo ni kuona taasisi hizo zinafanya uwekezaji mzuri kwa maslahi ya Taifa kwani ndio wenye jukumu la kutoa muongozo na kusimamia mali za umma katika taasisi hizo.

Ameongeza kuwa kazi yake kubwa ni kuruhusu kutumia au kuondolewa kwa mali za umma pamoja na kutoa muongozo utakaoelekeza namna nzuri ya kuongoza taasisi zao.

Washiriki wa mkutano huo waliahidi kutoa ushirikiano wao katika Ofisi hiyo sambamba na kukubaliana katika utendaji wa kazi zao.

Aidha, wanaomba kufahamu mikataba wanayoingia na Taasisi nyengine ili kujua muongozo husika wanaotakiwa kuutumia katika kazi zao.

Wameongeza kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina huweka mwongozo maalumu kwa taasisi zinazojiendesha kibiashara ili kuondosha changamoto zinazoweza kujitokeza na kuleta tija.







**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

# ZANZIBAR




**JARIDA LIMEANDALIWA NA**
**OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR**